Tambueni kuwa dunia imelaaniwa, na vimelaaniwa vilivyomo, isipokuwa kumtaja Mwenyezi Mungu na yanayompendeza, na msomi, au mwanafunzi

Imepokewa kutoka kwa Abuu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Nilimsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake akisema: "Tambueni kuwa dunia imelaaniwa, na vimelaaniwa vilivyomo, isipokuwa kumtaja Mwenyezi Mungu na yanayompendeza, na msomi, au mwanafunzi".

[Ni nzuri (Hasan)] [Imepokelewa na Tirmidhi na bin Majah]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kwamba dunia na vilivyomo inachukiwa mbele ya Mwenyezi Mungu na haipendezi bali imetengwa mbali, yameachwa yote yaliyomo hayasifiki kwa uzuri; kwakuwa dunia na vilivyomo hushughulisha na kuwatenga mbali watu na Mwenyezi Mungu Mtukufu, isipokuwa kumtaja Mwenyezi Mungu na kila kinachokaribia hilo na kuwa katika aina hiyo katika yale anayoyapenda Mwenyezi Mungu, au mwalimu wa elimu ya kisheria anayewafundisha watu, au mwenye kujifunza.

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3788